

Usalama wa Chanjo ya COVID-19: Jambo la Kujua



Chanjo ziko salama

Chanjo za COVID-19 tulizo nazo Marekani zimekuwa katika ufuatiliaji wa kina zaidi wa usalama katika historia ya Marekani¹. Chanjo zote ama zimeidhinishwa kamili kwa ajili ya matumizi ya na U.S. Food and Drug Administration (FDA, Usimamizi wa Chakula na Dawa Marekani)—kumaanisha kuwa FDA haikupata wasiwasi wowote wa usalama.

Chanjo zinaendelea kufuatiliwa kwa ajili ya usalama na ufaafu zinavyozidi kutumika kwa umma. Marekani ina mifumo kadhaa inayotumika kuangalia masuala ya usalama na kuyapata kwa haraka yakifanyika.



Chanjo inafanya kazi

Unaweza kuwa umeona maelezo yanayofanya ionekane kama baadhi ya chanjo ni bora kwa nyingine. Majaribio ya kimatibabu yalionyesha kuwa chanjo zote zinazopatikana zilifanikiwa zaidi katika kuzuia COVID-19. Tofauti kati ya chanjo ni ngumu kulinganisha kwa sababu zilipimwa katika wakati na maeneo tofauti. Baadhi yao zilipimwa hata dhidi ya aina tofauti za COVID-19.

Mara tu umepewa uchanjo kamili, bado inawezekana kupata COVID-19, lakini hutaweza kuwa mgonjwa zaidi na kuenda hospitalini. Utafiti ulionyesha kuwa kila chanjo ilikuwa na angalau ufaafu wa asilimia 85 katika kuzuia maradhi **makali** ya COVID-19 Chanjo pia ziliwazuia watu wengi dhidi ya kupata dalili **zozote** za COVID-19

- Johnson & Johnson (Janssen), asilimia 74
- Pfizer-BioNTech, asilimia 95
- Moderna, asilimia 94

Madhara haya ni za kawaida

Huwezi kupata COVID-19 kutokana na chanjo. Hata hivyo, sawa na chanjo nyingine, unaweza kuhisi madhara. Hizi ni dalili kuwa chanjo inafanya kazi. Kwa chanjo za dozi mbili, madhara baada ya sindano ya pili yanaweza kuwa hatari. Ikiwezekana, jipe muda wa kupumzika na kuwa sawa kwa siku moja au mbili baada ya kudungwa sindano ya chanjo. Kwa chanjo za COVID-19 zinazohitaji dozi mbili, hakikisha umepata dozi yako ya pili. Hutakuwa umelindwa kamili hadi wiki mbili kupita baada ya dozi yako ya pili.

Kwenye mkono wako katika eneo lililodungwa sindano:

- Maumivu
- Wekundu
- Kuvimba



KWenye mwili wako wote:

- Uchovu
- Maumivu ya kichwa
- Maumivu ya misuli
- Baridi kali
- Joto kali
- Kichefuchefu



¹Centers for Disease Control and Prevention, "Safety of COVID-19 Vaccines (Usalama wa Chanjo za COVID-19)". Machi 25, 2021, inapatikana mtandaoni katika: <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/safety/safety-of-vaccines.html>.



Dalili za mzio

Mizio ya chanjo ni nadra sana, lakizi inaweza kufanyika. Hospitali itakuangalia kwa angalau dakika 15 baada ya chanjo yako ikiwa utakuwa na mzio. Wamefunzwa kushughulika na kujua jinsi ya kukusaidia.

Ukiwa na mzio baada ya kuondoka kwenye kliniki, piga 911. Dalili za mzio zinajumuisha: matatizo ya kupumua, kuvimba kwa uso wako na koo yako, mdundo wa haraka wa moyo, upele mbaya mwilini wako wote, kizunguzungu na udhaifu.

Tusaidie kufuatilia wasiwasi wowote wa usalama




Jisajili kwa V-safe ili kuripoti madhara yoyote: v-safe.cdc.gov. Ushiriki wako hutusaidia kuweka chanjo salama kwa kila mtu.

Wewe au mtoaji wa chanjo yako anaweza kuripoti madhara makali kwenye the Vaccine Adverse Event Reporting System (VAERS, Mfumo wa Kuripoti Tukio Hatari ya Chanjo). FDA, Centers for Disease Control and Prevention (CDC, Vituo vya Udhhibiti na Uzuiaji wa Ugonjwa) na Washington State Department of Health (DOH, Idara ya Afya) ya Jimbo la Washington hutumia VAERS kufuatilia mielekeo au matatizo yanayowezekana.

Unaweza kuwasilisha ripoti katika vaers.hhs.gov.

Watu wa asili na makabila mengi yalishiriki katika majaribio

Wanasayansi walipima kila chanjo kwa maelfu ya watu.



²Food and Drug Administration. "FDA Briefing Document: Pfizer-BioNTech COVID-19 Vaccine", Mkutano wa Vaccines and Related Biological Products Advisory Committee (Kamati ya Ushauri wa Chanjo na Bidhaa za Kibiolojia Zinazohusiana na Chanjo). Desemba 10, 2020, inapatikana mtandaoni katika: <https://www.fda.gov/media/144245/download>.

³Food and Drug Administration. "FDA Briefing Document: Janssen Ad26.COVID.S Vaccine for the Prevention of COVID-19", Mkutano wa Vaccines and Related Biological Products Advisory Committee. Februari 26, 2021, inapatikana mtandaoni katika: <https://www.fda.gov/media/146217/download>.

⁴Food and Drug Administration. "FDA Briefing Document: Moderna COVID-19 Vaccine", Mkutano wa Vaccines and Related Biological Products Advisory Committee. Desemba 17, 2020, inapatikana mtandaoni katika: <https://www.fda.gov/media/144434/download>.



Chanjo hiyo ni salama na faafu kwa watoto, wajawazito, na walio na hali za kiafya. Watu zaidi wanavyozidi kupokea chanjo, tutaendelea kupata data zaidi kuhusu usalama na madhara. Data zinaonyesha kuwa chanjo za COVID-19 ziko salama, na madhara makali ni nadra.

Ongea na mhudumu wa afya au mfanyakazi wa kliniki ikiwa una masuala kuhusu kupata chanjo



Mizio

- Centers for Disease Control and Prevention (CDC, Kituo cha Udhambi na Uzuiaji wa Ugonjwa) inapendekeza chanjo kwa mtu yeyote ambaye hana mzio wa viambato vyovyote vya chanjo hiyo.
- Mizio ya chanjo ya COVID-19 mara kwa mara hufikiriwa kusababisha na mafuta yaliyo kwenye chanjo, yanayoitwa polyethylene glycol (PEG) na polysorbate.
- Chanjo hazina vitu sawa vya kusababisha mzio kama vile vinavyopatikana kwenye chakula, hivyo mizio mingine zaidi haifai kuwa wasiwasi wakati wa kupata chanjo ya COVID-19. Kwa mfano, chanjo hazina mayai, hazina ulimbo wa mpira, na hazina vifaa vya kuhifadhi.

Maadili

Viambato vya chanjo ya COVID-19 ni salama na vinahitajika kwa chanjo kufanya kazi yao. Kipande kimoja cha chanjo ya Johnson & Johnson kimeundwa ndani ya nakala za seli zilizoundwa ndani ya maabara ambazo asili yao ni mimba ya kuavya iliyofanyika zaidi ya miaka 35 iliyopita. Chanjo nyingine nyingi, ikijumuisha tetekuwanga, surua, na homa ya manjano A, zimeundwa kwa njia sawa. Hakuna chanjo iliyo na seli za binadamu (ikijumuisha seli za kijusi), virusi vya COVID-19, mpira, vifaa vya kuhifadhi, au bidhaa yoyote kutoka kwa mnyama ikijumuisha bidhaa za nyama ya nguruwe. Chanjo hizi hazikuzwi kwenye mayai na hazina bidhaa za mayai.

Hali za Kiafya

- Utafiti ulionyesha kuwa chanjo za COVID-19 zilikuwa tu salama na faafu kwa watu walio na hali za kimatibabu. Asilimia ishirini hadi 45 ya washiriki katika kila majaribio ya chanjo walikuwa na hali kama unene wa kupita kiasi, kisukari, ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa ini, na VVU.
- Tuna data chache ya usalama kuhusu utumiaji wa chanjo katika watu walio na mifumo dhaifu ya kinga au hali za kinga otomatiki. CDC bado inapendekeza chanjo kwa vikundi hivi kwa sababu vina hatari ya juu ya magonjwa hatari wakipata COVID-19.
- Wataalamu wa matibabu katika ujauzito na uzazi wanapendekeza chanjo ya COVID-19 kwa watu ambao ni wajawazito, wanaonyonyesha, au wanapanga kuwa wajawazito. Data inaonyesha kuwa chanjo za COVID-19 ziko salama wakati wa ujauzito. Kwa kweli, baadhi ya utafiti unaonyesha kuwa mzazi aliyepewa chanjo anaweza kata kupitisha kingamaradhi dhidi ya COVID-19 hadi kwa mtoto wao kupitia ujauzito na kunyonyesha. Watu wajawazito wapo hatarini ya magonjwa makali dhidi ya COVID-19, ikijumuisha hadi kifo. Chanjo ndizo ulinzi bora.